



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA BUKOBA  
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. KGR/BDC/S.2/70/105

21/03/2022

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba anawatangazia nafasi za kazi Madereva wawili (2) na Wasaidizi wa Hesabu wawili (2) ajira ya Mkataba raia wote wa Tanzania wenye Sifa za kujaza nafasi hizo kwa sifa zinazooneshwa hapa chini:-

### (I) DEREVA II – (NAFASI 02) – TGS B.

#### SIFA ZA MWOMBAJI

- ❖ Awe na Elimu ya Kídato cha IV au cha VI.
- ❖ Awe na leseni daraja la E au C 1 ya uendeshaji wa magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja(1) bila kusababisha ajali.
- ❖ Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari(Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha mafunzo ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- ❖ Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi daraja II watafikiriwa kwanza.

#### MAJUKUMU YA KAZI

- ❖ Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- ❖ Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- ❖ Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
- ❖ Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
- ❖ Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
- ❖ Kufanya usafi wa gari pamoja na kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake.

### (II) MSAIDIZI WA HESABU II – (NAFASI 2) – TGS B

#### SIFA ZA MWOMBAJI

- ❖ Awe na elimu ya kidato cha IV au cha VI.
- ❖ Awe na cheti cha ATEC Level Ikinachotolewa na NBAA au sifa nyingine zinazolingana na hizo zinazotambulika na NBAA.
- ❖ Awe na Cheti/ Astashahada ya Uhasibu kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.


## MAJUKUMU YA KAZI

- Kuandika na kutunza "**Register**" zinazohusu shughuli za Uhasibu.
- Kuandika hati za malipo na hati za mapokezi ya Fedha.
- Kutunza majalada yenye kumbukumbu za Hesabu.
- Kupeleka barua/nyaraka za Uhasibu Benki.
- Kufanya usuluhishi wa Masurufu, Karadha, Hesabu za Benki na Amana.

## MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

1. Mwombaji awe ni raia wa Tanzania na mwenye umri wa miaka kuanzia 18 na kuendelea.
2. Mwombaji aambatishe nakala ya Cheti cha Kuzaliwa.
3. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo binafsi (CV), nakala za vyeti vya kidato cha nne au kidato cha sita kwa wale waliofika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa.
4. Picha moja Passport Size iandikwe jina kwa nyuma.
5. Hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (**Statement of Results**)havitakubalika.
6. **Ajira hii ni ya Mkatoba wa miezi kumi na mbili (12). Mkatoba waweza kuongezewa kwa kutegemeana na uwezo wa mtumishi wa kufanya kazi.**
7. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya kiingereza au Kiswahili na yatumwe kwa njia ya Posta kabla ya tarehe **01/04/2022**kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya,  
S.L.P 491,  
**BUKOBA.**

  
Fatima H. Laay  
**MKURUGENZI MTENDAJI WAWILAYA  
HALMASHAURI YA WILAYA BUKOBA  
MKURUGENZI MTENDAJI**

Nakala kwa: Ubao wa Matangazo,  
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,  
S.L.P 299,  
**KAGERA.**

" " Ubao wa Matangazo,  
Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,  
S.L.P 9,  
**BUKOBA.**

" " Ubao wa Matangazo,  
Halmashauri ya Manispaa  
**BUKOBA**

---

Sanduku la Posta 491 Bukoba, Kagera

Simu: 028 2220287, nukushi: 028 2221839 barua pepe: [dad@bukobadc.go.tz](mailto:dad@bukobadc.go.tz), tovuti: [bukobadc.go.tz](http://bukobadc.go.tz)